BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 24 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

67. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Ni kwa kiwango gani Serikali imetathmini utekelezaji wa hoja zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

### Wizara ya Fedha na Mipango:

112. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

    Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni benki ya watu wa Zanzibar ambayo kwa kiasi kikubwa inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

    (a) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inaitumia benki hii.

    (b) Je, ni kwa nini miamala mingi ya kiserikali inafanyika bila ya

kuitumia PBZ.

(c) Je, ni tatizo gani hasa linaloifanya Serikali kutoitumia kiukamilifu benki hii ya kizalendo.

**<u>Wizara ya Kazi na Uwekezaji:</u>**

12. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Je, Serikali imechukua hatua zipi za kuondoa vikwazo vinavyowakabili wawekezaji kama vile urasimu, upungufu wa miundombinu na gharama za uzalishaji ili kuhamasisha zaidi uwekezaji Zanzibar.

82. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Uwekezaji ni jambo muhimu sana sio tu kwamba unasaidia kuongeza mapato ya Serikali lakini pia husaidia kupunguza changamoto kubwa ya ajira.

Je, ni kwa kiasi gani ongezeko la wawekezaji limesaidia kutatua au kupunguza changamoto ya ajira hasa kwa vijana hapa Zanzibar.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

88. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Kengeja Sekondari ni miongoni mwa skuli kongwe nchini ambayo imejengwa mwaka 1922. Kutokana na ukongwe wake, skuli hiyo hivi sasa ni mbovu, inavuja na hata madarasa yake ya kusomea hayatoshi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuikarabati ama kuijenga upya skuli hiyo katika kiwango cha ghorofa.

134. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na changamoto kubwa kwa watoto wanaoendelea na masomo yao katika skuli ya Miti Ulaya Wete, wanaotokea katika Kisiwa cha Mtambwe Mkuu jimbo la Mtambwe. Watoto hawa hulazimika kuvuka kwa vidau ambavyo si salama kwani wanakosa chombo chenye usalama.

(a) Je, Wizara inaifahamu vipi changamoto hii inayowakumba watoto wa kisiwa cha Mtambwe Mkuu.

(b) Ni lini Serikali inapeleka *Fiber Boat* yenye usalama kwa ajili ya kuwasafirisha watoto hawa hususan wa madarasa ya juu ambao hayapatikani katika Skuli ya Maandalizi.

**Wizara ya Mawasiliano,Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

109. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kwa kuwa usajili wa simu ni lazima kwa wananchi wote ili kuweza kudhibiti uhalifu.

(a) Je, kwa nini vitendo vya kutuma ujumbe (sms) wa kitapeli vinaendelea kuongezeka kupitia simu za wananchi wetu.

(b) Je, kesi ngapi za kitapeli kupitia ujumbe wa simu zimeripotiwa na kuchukuliwa hatua.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

148. MHESHIMIWA MIHAYO JUMA SULEIMAN (Jimbo la Mwera) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwepo na malalamiko ya wananchi ya kusomeka vyombo vyao vya usafiri katika mifumo ya maegesho ya magari ya mjini kuwa wanadaiwa ada ya maegesho hali ya kuwa vyombo hivyo havijaenda mjini kwa tarehe hizo zilizomo katika mtandao wao.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua madhubuti za ukusanyaji wa mapato wa maegesho kwa utaratibu uliokuwa mzuri bila ya usumbufu.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

27. MHESHIMIWA AZA JANUARY JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

    Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua kubwa ya maendeleo katika ujenzi wa barabara mijini na vijijini.

    a) Kwa nia ya kuzitunza barabara zetu, ni utaratibu gani uliowekwa wa kuzitumia barabara hizo kwa magari makubwa ya mizigo.

    b) Ni upi mkakati wa Serikali wa kuzijenga barabara za ndani zilizopo vijijini.

120. MHESHIMIWA MARIAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

    Wananchi wa shehia ya Kengeja wanaojishughulisha na ufugaji, kilimo pamoja na uchumaji wa zao la karafuu, hulitumia zaidi daraja la Bopwe katika kuendeleza shughuli zao za kiuchumi. Hata hivyo, daraja hili kwa sasa ni bovu na unapofika wakati wa kipindi cha mvua, wananchi hao hushindwa kupita katika daraja hilo.

    Je, Serikali ina mpango gani wa kulijenga daraja hilo ili kurahisisha mawasiliano kwa wananchi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

144. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Pamoja na Idara ya Misitu kuwa ni muhimu katika ukusanyaji wa mapato ya Wizara, majengo yake ni chakavu na hayafanyiki hata matengenezo (repair), huku watumishi wa Idara hiyo wakikabiliwa na upungufu pamoja na uchakavu wa vyombo vya usafiri.

    Ni lini Serikali itaanza utaratibu wa kujenga majengo mapya ya kisasa kwa Idara ya Misitu Wete na kuipatia vyombo vipya vya usafiri.

247. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wakala wa Matreka umepewa jukumu la kuagiza matrekta kwa ajili ya kutoa huduma za kuwalimia wakulima wa mpunga.

(a) Je, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ni matrekta mangapi yameagizwa.

(b) Je, katika kipindi hicho, kuna matrekta mangapi yamewahudumia wakulima wetu.

**Wizara ya Afya:**

3. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi, hasa maeneo ya vijijini ambapo upatikanaji wake bado ni mdogo.

66. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni kwa nini baadhi ya dawa muhimu za magonjwa ya kibinaadamu zinakosekana katika hospitali za Serikali lakini zinapatikana kwa wingi kwenye hospitali na maduka binafsi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

91. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa maji ni jambo muhimu sana kwa maisha ya binaadamu na viumbe mbalimbali vyenye uhai. Na kwa kuwa shehia za Ndagoni katika jimbo la Ziwani zimekuwa na tatizo sugu la maji safi na salama kwa kipindi kirefu, jambo linaloleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Je, ni lini Serikali italipatia suluhisho tatizo hilo sugu la wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

55. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Katika kila mwaka kuna siku 16 za kupinga ukatili na udhalilishaji ambazo Serikali yetu imekuwa kinara na kuzitumia vizuri siku hizo kupiga vita masuala yote yanayohusu ukatili na udhalilishaji wa wananchi wake.

(a) Je, kuna tafiti zozote zilizofanyika ili kujua mafanikio na changamoto juu ya jambo hili.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani katika kudhibiti udhalilishaji wa watoto kwa njia ya omba omba.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

159. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha Sekta ya Uvuvi kwa kuwawezesha wavuvi wa Zanzibar kwa kuwapatia boti, zana za kisasa za uvuvi na nyenzo nyengine muhimu, kwa lengo la kuongeza uzalishaji, kipato chao na mchango wa sekta hiyo katika uchumi wa taifa.

(a) Kwa kuzingatia hatua ilizozichukuwa kuwawezesha wavuvi wa Zanzibar, je, Serikali imefanya tathmini ipi ya kina ya kuimarika kwa Sekta ya Uvuvi.

(b) Ni kampuni ngapi za uvuvi zinazotokana na programu ya uwezeshaji zimesajiliwa na kupewa vibali vya kuvua katika Bahari Kuu

II. MATOKEO YA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA UMOJA WA WAWAKILISHI WANAWAKE ZANZIBAR (UWAWAZA) NA CHAMA CHA WABUNGE WANAWAKE WA NCHI ZA JUMUIYA YA MADOLA KANDA YA ZANZIBAR (CWP).

III. CHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA CHA WABUNGE WA NCHI ZA JUMUIYA YA MADOLA, KANDA YA ZANZIBAR (CPA).

Zanzibar,
24 Februari, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR